

Ukweli wa Injili

Mafundisho ya Biblia na Himizo
kwa Kaziya Kimisheni Ulimwenguni Kote

NGUVU ZINAZOTOKANA NA KUMSIFU MUNGU

Mfalme wa Yuda aliyejulikana kama Yehoshafati alisujudu mbele yake Bwana kwa maombi na kujinyima chakula. Kama ambavyo inakiliwa katika Kumbukumbu la Nyakati wa Pili, sura ya 20, kundi kubwa la maadui wa Yuda walikuwa wamekusanyika ili kufanya vita na Yehoshafati. Naye Yehoshafati, huku akiwa amejaa hofu nyingi kwa kujua kwamba watu wake hawangeweza kushinda adui huyo kwa nguvu zao wenyewe akamlilia Mungu na kusema: “Ee BWANA, Mungu wa baba zetu, si wewe uliye Mungu mbinguni? Tena si wewe utawalaye falme zote za mataifa? Na mkononi mwako mna uweza na nguvu, asiweze mtu ye yote kusimama kinyume chako . . . Maana sisi hatuna uwezo juu ya jamii kubwa hii, wanaotujia juu yetu; wala hatujui tufanyeje; lakini macho yetu yatazama kwako.” Naye Bwana akamjibu na kumwambia: “Msiogope, wala msifadhaika kwa ajili ya jeshi kubwa hili; kwani vita si yenu bali ni ya Mungu . . . hamtahitaji kupigana vita, jipangeni, simameni, mkaone wokovu wa BWANA ulio pamoja nanyi.”


Asubuhi iliyofuata, huku akiwa amejaa imani na ujasiri katika neno lake Mungu Yehoshafati alichagua waimbaji ambao walienda mbele ya jeshi lake huku wakitoa sifa kuhusu uzuri na utakatifu wake Mungu: “kwa maana fadhili zake ni za milele.” Na walipoanza kuimba na kumsifu, Bwana aliweka waviziao dhidi ya adui hao wakauawa na kuwaharibu. Basi Mungu akapatia watu wake ushindi mkubwa. Badala ya manunguniko kwa ajili ya woga na kukata tamaa kutokana na hatari ambayo ilikuwa imewakumba, wao waliweka imani na tumaini lao kwa Bwana na kumwambia na kumsifu.

Kuna nguvu nyingi ambazo hupatikana kutokana na mtu kumsifu Bwana. Adui yetu

hushindwa wakati Mungu amepewa heshima zake na ibada. Kuna vita vingi vya kiroho ambavyo ushindi wake umepatikana wakati watu wa Mungu waliinua mioyo yao na sauti zao kumsifu Bwana. Mkristo akimsifu Bwana kwa kupaza sauti, ushuhuda, na nyimbo, hayo yote hufungua malango na kumwezesha mtu kufika kwenye uwepo wake Mungu, kwa maana Yeye hudumu katika sifa za watu wake (Zaburi 22:23). Wakati wewe unapambana na Goliathu na hata kuta za Yeriko maishani mwako, huo ndio wakati unaofaa wa kumsifu Mungu ili uone nguvu na uwezo wake. Hebu kumbuka kwamba wana wa Israeli walizunguka kuta za Yeriko huku wakiwa na kimya kingi kwa muda wa siku sita. Lakini katika siku ya saba wakazunguka kuta za mji huo mara saba. Na katika mara hiyo ya mwisho kwa amri yake Bwana wana wa Israeli walipaza sauti, makuhani wakapiga tarumbeta zao, kwa maana Bwana alikuwa amewapatia mji huo. Basi walipopaza sauti zao kuta za mji wa Yeriko zikaanguka chini na wakanyakua mji huo (Yoshua 6:16-20). Bwana asifiwe! Lakini siku hizi watu wengine hata hawatoi neno la kimoyomoyo la kumshukuru Mungu, halafu baadaye wao hushangaa ni kwa nini kuta zinazowanyima ushindi maishani mwao hazianguki! Upasaji (wa kweli) wa sauti ya kiroho ni ile sauti ambayo hutoka ndani ya moyo wa mtu, sauti ambayo inatokana na Roho wake Mungu. Kwa kweli Bwana ni mkuu na anastahili kupewa sifa nyingi.

Kumsifu Bwana kwa njia ya imani wakati Mkristo anapitia giza kuu maishani mwake ni jambo ambalo humletea mabadiliko. Kumsifu Bwana humsaidia mtu kuwaza kumhusu Mungu badala ya kuwaza kuhusu udhaifu wa nafsi yake mwenyewe; anaacha kuwaza kuhusu hali yake ya kimwili dhidi ya vita ambavyo

(Inaendelea kutoka ukurasa 2)



“Mkristo akimsifu Bwana kwa kupaza sauti, ushuhuda, na nyimbo, yote hayo hufungua malango na kumwezesha mtu kufika kwenye uwepo wake Mungu, kwa maana Yeye hudumu katika sifa za watu wake.”

Tahariri

Mafundisho ya Biblia:
Sifa

Na Tumsifu Bwana

Maswali na Majibu

Je, Wajua?

3

4

5-6

7

Neno Linalofaa kwa
Msimu Huu

8

MAMBO AMBAYO BIBLIA INAFUNDISHA KUHUSU...

Neno la Mungu

2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35

Uhusiano wa Upendo

Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, 1 Yoh. 4:7-21

Toba

Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10

Uzao Mpya

Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4,
Efe. 2:1, 5-6

Uhuru Kutokana na Dhambi

1 Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11

Ujazo wa Roho Mtakatifu

Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8

Utakatifu

Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, 1 Pet. 1:15-16,
Tit. 2:11-12, Rum. 6:22

Ufalme wa Mungu

Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36

Kanisa

Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, 1 Kor. 12:12-13,
Kol. 1:18

Umoja

Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4

Kanuni za Kanisa

Mt. 28:19-20, 26:26-30, I Kor. 11:23-27,
Yn. 13:14-17

Uponyaji wa Kiungu

Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16

Utakatifu wa Ndoa

Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3,
I Kor. 7:10-11

Urembo wa Nje

I Tim. 2:9-10, I Kor. 11:14-15, Kum. 22:5

Mwisho wa Nyakati

2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10,
Mt. 25:31-46

Kupenda Amani

Lk. 6:27-29, 18:20

Ibada

Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17


Wajibu Mkuu

Mk. 16:15

(Endelea kutoka ukurasa 1)

anakumbana navyo. Sifa hizo humrudishia mtu hali ya kumwaza Yeye ambaye anaweza kutenda mambo yote. Wakati mtu amekufa moyo na kupatwa na misukumo mingine maishani, kumsifu Mungu hufungua lango la Mbinguni; na moyo wa mtu huyo unapata kuhuishwa tena na nafsi yake inapata uhai mpya.

Katika Matendo 16:22-26 Paulo na Sila walipigwa mijeledi (mingi) kwa njia ambayo haikuwa ya haki, wakatupwa gerezeni, na hata miguu yao ikafungwa kwa mkatale. Kwa kweli watu hawa wawili walikuwa na haki ya kunungunika na kuwa na kinyongo. Matokeo ya shauku lao la kuhubiri Injili na kumfanyia



“Wakati mtu amekufa
moyo ... kumsifu
Mungu hufungua lango
la Mbinguni; na moyo
wa mtu huyo unapata
kuhushwa tena na nafsi
yake inapata uhai mpya.”

Mungu kazi ilikuwa wao kupatwa na giza kuu, wakatokwa na damu, wakapatwa na uchafu, wakashikwa mateka, na hata wakapatwa na maumivu mengi. Lakini usiku huo wa manane, badala ya wao kulia machozi ya majuto na upweke, walianza kuomba na kuimba kumsifu Bwana. Maombi yao hayakuwa ya kujihurumia bali yalikuwa ya shukrani na ushindi, kama ambavyo inaonekana kupitia kwa wimbo ambao waliimba. Mwanzoni wao walionekana kwamba wameshindwa, lakini badala yake wakapata ushindi mioyoni mwao kutokana na wao kumtukua Mungu kwa njia ya sifa. Wao walitambua kwamba hata katika mateso na uchungu ambao walihisi, Yesu alikuwa angali anastahili kutukuzwa kama Bwana wa mabwana, na Mfalme wa wafalme. Usiku ulikuwa na giza tofauti lakini furaha ya Bwana ilikuwa ndio nguvu zao. Wakati wakiimba nyimbo hizo nzuri za sifa ndipo ushindi ukatokea kwa njia ya mtetemeko wa ardhi na gereza likianza kutetemeka. Nayo milango ya gereza ikafunguka na minyororo ambayo kila mfungwa alikuwa amefungwa ikaanguka. Basi ukombozi wao ukapatikana kutokana na kusifu.

Ewe mtoto wa Mungu, hebu inua kichwa chako na umpe Mungu sifa zake. Kamwe usitumaini mambo yanayoonekana, bali mtumaini Yeye ambaye ana nguvu zote mbinguni na duniani. Haijalishi giza ni ya aina gani ambayo inakukumba, haijalishi ukuta ni mrefu kiasi gani, haijalishi mteremko wa mlima ni hatari kwa kiwango kipi, na hata haijalishi bonde lina kina kikubwa vipi; haijalishi nguvu za moto ni za kiwango gani, na haijalishi majaribu unayopata ni makali kwa kiwango kipi, hebu wewe mtazame Yesu, hebu msifu Bwana. Hebu msifu kwa ajili ya wokovu wake. Msifu kwa ajili ya rehema zake. Msifu kwa ajili ya wema na upendo wake. Nguvu zake Mungu hufanya kazi kupitia kwa sifa za watu wake, hata wakati ambapo kuna dhoruba kali maishani. Kumsifu Mungu hufungua mweke wa nguvu zake Mungu kudhihirika kwa njia kuu zaidi. Haijalishi jinsi wajihisi kindani, hebu mtukuze Bwana kwa shukrani na sifa za kweli za kutoka moyoni mwako. Hebu mwimbie na upaze sauti kwa ajili yake Bwana, na utamwona adui akishindwa. Hebu tumsifu Bwana! ■

Gazeti la *Ukweli wa Injili* ni jalida ambalo linatolewa kila robo ya mwaka kwa manufaa ya Kanisa la Mungu kwa ajili ya mafundisho na kwa ajili ya kuwahimiza Wakristo ili washike kweli za Biblia. Tutembelee katika tovuti yetu ya www.thegospeltruth.org na ujiandikishe ili uwe ukitumiwa notisi kwa njia ya barua pepe kila wakati jalida hili likiwa tayari ili uweze kupata toleo la kila kipindi. Gazeti hili la *Ukweli wa Injili* linachapishwa katika nchi nyingi ili lisambazwe katika nchi hizo. Kazi hii inawezekana kupitia kwa matoleo yanayotolewa kwa hiari. Pia wewe ukitaka unaweza kutumiwa risiti ya vile tumelipa ushuru kutokana na zawadi yako.

—Mhariri, Michael Smith

Gospel Truth, P.O. Box 2042, Nixa, MO 65714 USA
editor@thegospeltruth.org

Tahariri



Maana fadhili zako ni njema kuliko uhai; midomo yangu itakusifu.
—Zaburi 63:3

Somo la muhula huu linashughulikia swala la kumsifu Mungu. Hata ingawa kumsifu Mungu ni amri kutoka kwa Mungu – ukweli ni kwamba, kumsifu Mungu ni mweke mkubwa ambao tumepewa, na ambao ni wa heshima kuu. Mungu ametutendea mambo mengi, je, tunawezaje kukosa kumrudishia mkono wa shukrani kwa kumtukuza kwa sauti za midomo yetu? Mioyo yetu inahitaji kujaa sifa hata katika wakati ambapo tunapitia ugumu maishani; nayo midomo yetu inahitaji kumsifu Bwana.

Kuna maandiko mengi yanayohusiana na somo hili, hivi kwamba hamna nafasi ya kutaja maandiko hayo yote katika toleo hili. Ni jambo la kushangaza kwamba hata ingawa kuna masomo mengi ambayo yamefundishwa kuhusu kumsifu Mungu, kungali kuna washirika wengi wa dhehebu la utakatifu ambao huonelea kwamba kumsifu Mungu ni jambo ambalo Mkristo anaweza kujiamulia mwenyewe kufanya au kutofanya. Hata hivyo wengi wa washirika wa kanisa hili huwa wameshika mafundisho kidogo kuhusu somo hili ambayo yametokana na sehemu mbili au tatu tu za biblia.

Wakati mwingi wa kusifu ambao mimi mwenyewe nishawahi kuwa nao, na ambao ulikuwa wa kupendeza sana ulikuwa kati yangu peke yangu na Bwana, nikiwa pale ofisini au nikiendesha gari barabarani. Lakini ukweli wa mambo ni kwamba, mimi tayari nishawahi kujaribiwa mara nyingi kuzima sifa hizo za kibinafsi kwa kisingizio kwamba nitamsifu Bwana tukiwa katika ushirika na Wakristo wale wengine. Basi hebu sote tusimame wima dhidi ya mipango ya adui yetu ambaye anajaribu kuzima sauti ya sifa zetu kwake Bwana.

Kuna makusanyiko ya kanisa ambayo wakati mmoja au mwingine yalikuwa na uhai mwingi, yakawa yamejaa roho wa kumsifu Mungu, lakini kwa sasa makanisa hayo yamekuwa yenye unyamavu mkubwa, makanisa yaliyochoka kabisa. Lakini Mungu anataka watu wake wawe na ari ya kutafuta mapenzi yake. Kusema kweli maneno matupu hayana umuhimu yakilinganishwa na maisha ya utakatifu, lakini pia sisi tumeamurishwa kwamba tuwe na matamshi ya kusema kuhusu maisha ya Kikristo ambayo yanaendelea ndani mwetu. Kwa kweli kutakuwa na nyakati za kumwabudu Mungu kwa njia ya kimoyomoyo, lakini pia kutakuwa na nyakati za furaha kuu tunayohitaji kuitamka. Wakristo wengi wameanza kupungukiwa na viwango vilivyowekwa na Biblia kuhusiana na jinsi ambavyo tunahitaji kuishi maisha yetu, kama watu walio na wajibu wa kumsifu Bwana. Lakini tendo hilo la kumsifu Mungu silo jambo ambalo huanza katika ibada ya kanisa, bali linaanza katika maisha ya kibinafsi ya ushirika kati ya Mkristo na Bwana wake.

Sifa za kweli sio zile za kulazimishwa au kusukumwa ili kujionyesha kwamba mtu anashiriki ibada ya pamoja, bali ni tendo la mtu kujiamulia, tendo linalotoka moyoni mwa Mkristo. Bwana angependa kwamba kwa nguvu za Roho wake tukuze hali maishani mwetu ambayo inafaa kwa ajili ya kazi yetu ya kumsifu.

Hebu basi tumwombe Mungu ili Yeye atuwezesha kuwa waaminifu kwa ajili ya wajibu wetu wa kumsifu, kwa maana kulingana na kiwango ambacho tunamtukuza ndivyo ambavyo roho zetu zitaweza kubarikiwa.

Michael W. Smith

Oktoba 2019.

KUINUA MIKONO MITAKATIFU

Kwa jina lako nitaiinua mikono yangu. – Zaburi 63.4

Imekuwa ni mazoea ya watu wa Mungu tangu nyakati za Agano Jipya na Agano la Kale kuinua mikono wanapomwomba Mungu na kumsifu. Jambo hilo linapofanyika katika maombi hii huwa ni ishara ya unyenyekevu na hali ya mtu kuwa mhitaji mbele yake Yeye ambaye hutupatia vitu vyote, na mikono hiyo huwa ni ishara ya kumwomba na kumtegemea Bwana. Lakini wakati mtu anapofanya sifa tendo la kuinua mikono huwa ni dhihirisho ya heshima na hali ya mtu kunyenyekea mbele zake Mwokozi wetu na Baba yetu wa Mbinguni.

Wakati nyimbo za Sayuni zinapoimbwa mikono iliyoinuliwa huwa ni kuonyesha sifa na heshima ambazo tunatoa kwake Bwana; pia huwa ni ishara ya kukubali, ishara ya ombi la mhitaji, jambo la kuonyesha mtu aliye na shauku na tamaa sana kwa kile ambacho anaimba au kusema kuhusu.



menge kwa mtandao

Tutembelee kwa

www.thegospeltruth.org

ili uagize na kusoma

jarida letu.

Mwongozo wa Kujifunza Biblia

Somo: SIFA

Somo la Maandiko: *Mfanyieni BWANA shangwe, dunia yote; Mtumikieni BWANA kwa furaha; Njoni mbele zake kwa kuimba; Ingieni malangoni mwake kwa kushukuru; Nyuani mwake kwa kusifu; Mshukuruni, lihimidi. —Zaburi 100:1-2, 4.*

Maana: Kusifu ni tendo la kukubaliana na kitu, kufurahishwa nacho, au kukusifu. Hili ni tendo la kuabudu kwa kutumia maneno au wimbo, jambo ambalo huleta utukufu na heshima kwa yule ambaye anapewa sifa hizo.

Muhstasari: Mungu anastahili sifa na heshima zote. Sio eti kwamba watu wa Mungu wana wajibu wa kumwabudu tu, bali hasa wao wana mweke mkubwa waliopewa wa kumtukiza kila wakati kwa sifa na kwa nyimbo. Sifa za kweli huwa hazitokani na kimwili, bali hutoka kwa roho, na pia kunatokana na mtu kuishi maisha matakatiifu. Kuna nguvu zinazopatikana kutokana na Mkristo kumsifu Mungu, kwa maana sifa hizo hufungua malango na kumfikisha anayesifu katika uwepo wake na baraka zake (Mungu).

I. Amri ya Kumsifu Mungu

- A. Ufunuo 19:4-7 Watumishi wake wote.
- B. Warumi 15:9-11 Wito wa kufurahi na kusifu.
- C. Zaburi 117:1-2 Watu wote na mataifa yote.
- D. 1 Mambo ya Nyakati 16:23-36 Ni mkuu na anastahili sifa zote.
- E. Waebrania 13:15 Dhabihu ya sifa.

II. Kuimba na Kutoa Shukrani

- A. Zaburi 9:11 Tuimbe kwa sifa.
- B. Zaburi 107:1-2 Waliokombolewa waseme hivyo.
- C. Waefeso 5:19-20 Kuimba na kumshukuru Mungu.

III. Sababu ya Kusifu

- A. Luka 10:19-20 Majina yameandikwa Mbinguni.
- B. 1 Samueli 4:5-6 Uwepo wake Mungu.
- C. Zaburi 29:2 Utukufu wa jina lake.
- D. Yoeli 2:26 Mungu hukutana na mahitaji yetu.
- E. Zaburi 147:1 Yeye ni mzuri na ni wa kupendeza.

IV. Wakati Upi na Wapi

- A. Wafilipi 4:4 Furahini sikuzote.
- B. Zaburi 35:28 Mchana kutwa.
- C. 1 Petro 4:12-13 Katika majaribu, masumbufu, na mateso (Luka 6:22-23).
- D. Zaburi 149:1 Katika kusanyiko la watakatifu.
- E. Zaburi 150:1-2 Ulimwenguni kote.

V. Mfano wa Sifa

- A. Luka 18:42-43 Kipofu aponywa.
- B. Matendo 3:8-9 Kiwete aponywa.
- C. Luka 19:35-40 Wanafunzi wafurahi.
- D. Luka 23:44-49 Akida wa Kirumi.

VI. Sifa za Sayuni

- A. Isaya 60:18 Malango yaitwayo sifa.
- B. Zaburi 137:1-4 Uhamisho huzuia sifa.
- C. Isaya 35:8-10 Njia ya utakatifu.
- D. Isaya 61:3 Vazi la sifa.
- E. 1 Petro 2:9 Kutangaza fadhili za Bwana.
- F. Isaya 12:3-6 Kupaza sauti na kupiga kelele.

VII. Jinsi ya Kusifu na Kuabudu

- A. Yohana 4:21-24 Kwa roho na kweli.
- B. 1 Wathesalonike 5:16-19 Msizime Roho.
- C. Waebrania 12:28 Unyenyekevu na kicho.
- D. 1 Petro 4:10-11 Yesu anastahili sifa.
- E. Yoeli 2:26-27 Kusifu Bwana bila kuaibika (kutahayari).
- F. 1 Wakorintho 14:40 Vizuri na kwa utaratibu.

VIII. Sifa za Kweli na Sisizo za Kwali

- A. Isaya 29:13 Mioyo iliyofarakana na Mungu.
- B. Isaya 42:8-10 Mungu hampi mwingine utukufu wake.
- C. Zaburi 138:1 Kwa moyo wote.
- D. Wafilipi 3:3 Kutoutumaini mwili.

IX. Nguvu za Sifa

- A. 2 Mambo ya Nyakati 20:20-22 Yehoshafati.
- B. Yoshua 6:16 Vita vya Yeriko.
- C. Matendo 16:25 Paulo na Sila.

Tamati

*Kila mwenye pumzi na amsifu BWANA.
Haleluya. —Zaburi 150:6*





Na Tumensifu Bwana

Kumsifu Mungu kulingana na ukweli ni tendo la kiroho na pia ni tendo la kiibada. Kumsifu Bwana sio tu kurudia maneno hivi hivi, na pia silo jambo la kihisia tu; kumsifu Bwana ni tendo linalotokana na mtu kuamua kumtii Bwana, wakati mtu huyo anapotoa shukrani kwa Mungu kwa kumtukuza na kumsifu.

“Kama kuna sifa
na shukrani
moyoni, sifa na
shukrani hizo
zinahitaji kutoka
midomoni mwetu
kama sadaka
kwake Mungu.”

Amri ya Kumsifu Mungu

Kumsifu Mungu si jambo ambalo tumeshauriwa kufanya, bali ni amri ambayo imetolewa karibu mara 250 katika Biblia. Mfalme Daudi alikuwa mtu aliyependa kumsifu Bwana sana, na alikuwa amejifunza siri ya kukaribia uwepo wake Mungu. “Ingieni malangoni mwake kwa kushukuru; Nyuani mwake kwa kusifu” (Zaburi 100:4). Agizo la “Mtumikieni BWANA kwa furaha” na la “Njoni mbele zake kwa kuimba” (Zaburi 100:2) silo jambo tu linalopatikana katika Agano la Kale. Mungu hupata heshima na pia hutukuzwa kutokana na sifa na ibada inayotoka ndani ya mioyo ya watu wake; sifa hizo ni wajibu ambao mwanadamu amepewa. Wakristo wengi huwa na mtazamo kwamba kusifu ni jambo ambalo mtu huchagua kufanya au kutofanya kulingana na maumbile ya mtu. Lakini katika Ufunuo 19:5,7 Biblia inasema “Sauti ikatoka katika kile kiti cha enzi ikisema, Msifuni Mungu wetu, enyi watumwa wake wote . . . Na tufurahi, tukashangilie, tukampe utukufu wake; kwa kuwa arusi ya Mwana-Kondoo imekuja, na mkewe amejijweka tayari.” Nayo Warumi 15:10-11 inatilia mkazo amri hiyo ya watu WOTE wamsifu Mungu na pia kumpa shukrani.

Mungu Anastahili Sifa

“Haleluya. Enyi mataifa yote, msifuni BWANA, Enyi watu wote, mhimidini. Maana fadhili zake kwetu sisi ni kuu, na uaminifu wa BWANA ni wa milele” (Zaburi 117:1-2). 1 Mambo ya Nyakati 16:23-36 inatoa mfano bora wa jinsi Bwana alivyo mkuu na anavyostahili sifa zetu. Yeye ndiye muumba wa ulimwengu wote na anazo nguvu, heshima, na utukufu wote. Yeye ni mwema na rehema zake zadumu milele. Yeye ni Mungu wa wokovu wetu. Mstari

wa 29 unatwamuru kwamba: “Mpeni BWANA utukufu wa jina lake; leteni sadaka, mje mbele zake; mwabuduni BWANA kwa uzuri wa utakatifu.”

Dhabihu ya Sifa

Watu hujieleza kwa njia tofauti tofauti, lakini sifa ni dhabihu ambayo Mungu angali anataka tumtolee katika kipindi hiki cha neema. “Basi, kwa njia yake yeye, na tumpe Mungu dhabihu ya sifa daima, yaani, tunda la midomo iliungamayo jina lake” (Waebrania 13:15). Kama kuna sifa na shukrani moyoni, sifa na shukrani hizo zinahitaji kutoka midomoni mwetu kama sadaka kwake Mungu. Pengine litakuwa jambo ngumu mtu kusifu kwa sauti, lakini wakati mwingi maisha ya kumwishia Mungu huwa si jambo rahisi. Sifa zinazotokana na sauti ya kutoka moyoni mwa mtu ni jambo ambalo tumeamuriwa kufanya na ambalo pia hutuletea baraka za ajabu.

Sifa Za Kutumia Sauti

Sehemu moja ya sifa ni mtu kumtukuza Mungu kwa sauti: “Mshukuruni BWANA kwa kuwa ni mwema, kwa maana fadhili zake ni za milele. Na waseme hivi waliokombolewa na BWANA” (Zaburi 107:1-2). Sifa pia hutolewa kwa njia ya nyimbo, “Mwimbieni BWANA akaaye Sayuni” (Zaburi 9:11). Nayo Waefeso 5:19-20 inawaagiza watu wa Mungu kuimba na kumtolea shukrani kwa mambo yote.


Sababu za Kumsifu Mungu

Kuna sababu nyingi za kumsifu Mungu. Sifa kwa Mungu hazistahili kutegemea hali ambayo imetuzunguka, kwa sababu Mungu angali ni Mungu hata tunapopitia wakati mgumu maishani; Yeye anastahili sifa zetu. Yesu akawaambia wanafunzi

(Inaendelea kutoka ukurasa 6)

(Endelea kutoka ukurasa 5)

wake wafurahi kwa sababu “majina yenu yameandikwa mbinguni” (Luka 10:19-20). Msifu Bwana kwa maana anakutana na mahitaji yako na kukutunza (Yoeli 2:26). Wana wa Israeli nao “wakapiga kelele kwa sauti kuu, hata nchi ikavuma” (1 Samueli 4:5-6) wakati ule ambapo sanduku la agano la Bwana lilifika kambini. Hata sasa



mambo yanahitaji kuwa hivyo wakati uwepo wake Bwana unapokuwa miongoni mwa watu wake. Hapo kunastahili kuwe na furaha na kumsifu Bwana. Je, utakuwa ni ujuzi wa ajabu kiasi gani wewe kuwemo kati ya watakatifu ukimsifu Mungu kwa maneno na kwa nyimbo chini ya upako mkuu wa Roho Mtakatifu. “Haleluya. Msifuni Bwana; Maana ni vema kumwambia Mungu wetu, Maana kwapendeza, kusifu ni kuzuri.” (Zaburi 147:1). Kukosekana kwa sifa ambazo hazina mwisho kati ya watu wa Mungu linahitaji kuwa ni ishara ya kutuonya, kwa sababu Mungu hudumu kati ya sifa za watu wake.

“Sifa si jambo la kufanywa tu wakati wa ibada za kanisa, bali ni jambo ambalo linahitaji kuwa sehemu ya maisha yetu ya kila siku.”

Wakati wa Kusifu

Watu wa Mungu wanahitaji kufurahi ndani ya Bwana kila wakati (Wafilipi 4:4) na wanahitaji kuwa tayari kumsifu Bwana siku kucha (Zaburi 35:28).

Furaha hii haistahili kuweko tu wakati ambao unafaa, bali pia katika nyakati za majaribu makubwa, wakati mtu anapoumwa, na hata wakati wa mateso (1 Petro 4:12-13). Ni jambo la kushangaza jinsi ambavyo mwelekeo na roho ya mtu inaweza kubadilika wakati Mungu anapopewa utukufu na sifa. Sifa si jambo la kufanywa tu wakati wa ibada za kanisa, bali ni jambo ambalo linahitaji kuwa sehemu ya maisha yetu ya kila siku. Mungu anastahili kusifiwa kati ya umati (Zaburi 149:1) na katika hekalu ya viumbe vyote alivyounda (Zaburi 150:1-2). Sifa za kweli ni matamshi ya upendo ya kumwabudu Bwana ambayo yanatoka katika moyo ulio safi.

Mifano Kutoka kwa Biblia

Kuna michoro na mifano ya sifa inayopatikana kwenye hadithi ya kanisa la kwanza. Wakati Yesu alipomponya yule kipofu, mtu huyo alimtukuza Mungu na hata watu wale wengine “walimsifu Mungu” (Luka 18:42-43). Wakati yule kiwete alipoponya katika lango la hekalu, yeye alirukaruka na kumsifu Mungu (Matendo 3:8-9), akafurahi sana kwa jinsi ambavyo Mungu alimtendea jambo njema ndiposa yeye hakutembea tu, bali alirukaruka kwa furaha. Lakini moja ya hadithi ya sifa ambayo inavutia sana ni wakati Yesu aliingia jijini Yerusalemu huku akiwa amepanda mwanapunda: “kundi zima la wanafunzi wake walianza kufurahi na kumsifu Mungu kwa sauti kuu, kwa ajili ya matendo yote ya uwezo waliyoyaona” (Luka 19:37). Sauti hazikutoka tu kwa mtume Petro wakiwa

na wanafunzi wenzake ambao walipenda kuzungumza sana, bali watu wote walipatwa na furaha. Mafarisayo nao waliwakemea lakini Yesu akawajibu katika mstari wa 40: “Nawaambia ninyi, wakinyamaza hawa, mawe yatapiga kelele.” Je, ni nani atamsifu Bwana ikiwa watu wa Mungu hawatafanya hivyo? Je, watu wa Mungu wanastahili kuogopa kwamba wenzao hawatawaelewa wanapomsifu Mungu kwa sauti? Je, tutayaacha mawe kupiga kelele?

Sifa za Sayuni

Kuta za Sayuni (kanisa la Mungu) ni wokovu, nayo malango ya Sayuni ni sifa (Isaya 60:18). Wakati watu wanapitia malango ya sifa roho zao huinuliwa juu ya shida za maisha yao ya sasa na kuweza kufikia kwenye utukufu mkuu wa Yesu Kristo. Wao hufanywa kuwa kitu kimoja na sehemu ya utukufu wake Mungu. Lakini adui anapenda kufinyilia sifa za watu wa Mungu. Wakati wana wa Israeli walipokuwa uhamishoni Babiloni wao walitwika vinubi vyao kwenye miti iliyokuwa katikati huku wakilia na hawangeweza kuimba nyimbo za Sayuni (Zaburi 137:1-4). Lakini waliporudi Sayuni (kupitia kwa njia hiyo ya utakatifu) walifika huku wakiwa na nyimbo na furaha ya milele. Mambo yanastahili kuwa hivyo kati ya watu wa Mungu. Watakatifu “mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu” (1 Petro 2:9).

Sifa Zinazoongozwa na Roho

Yesu alifundisha kwamba “wamwabuduo yeye imewapasa kumwabudu katika roho na kweli” (Yohana 4:23). Sifa ambazo zinakubalika ni zile ambazo zinaongozwa na Roho Mtakatifu na kupata nguvu kupitia kwa maisha ambayo mwenye kuabudu anaishi kulingana na ukweli. Wakati sifa zinapojaa moyoni, tumeshauriwa kwamba “Msimzimishe Roho” (1 Wathesalonike 5:19), badala yake tunahitaji kufanya sifa zake Mungu kuvuma kutoka midomoni mwetu. Lakini katika ibada za pamoja, sifa za Kikristo sio zile za kuwafanya watu kuwa na hisia ambazo hazina vipimo, kwa maana sote tunahitaji kumwabudu Mungu kwa heshima na woga wa kiungu (Waebrania 12:28). Kila kitu kinahitaji kufanywa “kwa uzuri na kwa utaratibu” (1 Wakorintho 14:40), lakini pia kunahitaji kuwe na uhuru wa kumsifu Mungu bila kuona aibu (Yoeli 2:26-27). Yesu Kristo ndiye haswa tunastahili kusifu (1 Petro 4:10-11), lakini sifa hizo hazistahili kufanywa ili kuwatumbuiza watu au kuwa ni tamasha la kimwili (Wafilipo 3:3).

Nguvu Zinazopatikana Kutokana na Sifa Ambazo Zimekubalika

Wengi humwabudu Mungu kwa midomo yao ilhali mioyo yao iko mbali naye (Isaya 29:13). Lakini Mungu amekataa sifa za aina hiyo kwa sababu Yeye awatafuta wale wa kumsifu na kumpenda kwa mioyo yao yote. Hata ingawa zile ibada zinazofanywa katika mengi ya mashirika ya Kikristo huleta hasara kwa kanisa, hebu tusiruhusu adui yetu kuteka nyala au kuiba kile ambacho ni haki yetu kama watu wa Mungu. Kuna nguvu nyingi zizazopatikana kutokana na sifa za kibinafsi na za pamoja, naye Mungu hutukuzwa na kupewa heshima wakati watu wake wanapomwinua maishani mwao, katika mioyo yao, na pia kwa kutumia midomo yao. ■

Maswali na Majibu

Je, ikiwa mtu akinakili maandiko kutoka kitabu cha Zaburi wakati akijadili swala la kumsifu Mungu, na iwe kwamba yeye hatumii ala za muziki katika ibada za sifa kanisani mwake, je, huo utakuwa ni unafiki?

Hata ingawa Mfalme Daudi alikuwa mtu mwenye dhambi nyingi, maisha yake yalijaa sifa na ibada kwake Bwana. Kitabu cha Zaburi kimejaa maneno ya kumsifu Mungu. Yeye pia aliwahimiza watu wale wengine wamsifu Mungu, sio tu kwa nyimbo, bali pia nyimbo hizo zilandamane na ala za muziki, na hata kwamba mwenye kuabudu achez densi, kama inavyoonekana katika Zaburi 150. Mfalme Daudi aliishi chini ya himaya ya sheria ya Musa, na yeye hakujua ukweli wa Yesu Kristo. Basi kuna matendo na tabia za Daudi ambazo ni za kusifika na za kuvutia na hata za kutumika katika kipindi hiki cha neema.

Ukweli ni kwamba, si jambo la kinafiki mtu kunukuu kutoka kwa maadishi ya Daudi, na hata kutoka kwa wale manabii wengine wa kale wakati mtu akifunza, kuwajulisha, na kuwahimiza Wakristo. Lakini ikiwa kuna jambo ambalo liko kinyume na mafundisho ya Agano Jipya sisi basi hatufuati mfano huo. Hata ingawa sifa za Daudi zina mvuto mkubwa kwa sababu zingine zinalingana na mafundisho ya Agano Jipya, baadhi ya matendo yake hayakulingana na mafundisho na mazoea ya watakatifu wa Agano Jipya.

Daudi alitoa dhabihu kwa Bwana, akatoa fungu la kumi, na hata akaabudu kwa kutumia ala za muziki, lakini Wakristo wa kanisa la kwanza (la Agano Jipya) hawakufanya mambo hayo. Wao waliabudu kwa roho na kweli kinyume na matakwa ya kimwili na tamaduni za kisheria. Hakuna mafundisho katika Agano Jipya ambayo yanahimiza kuwe na matumizi ya ala za muziki katika ibada; zaidi ya hayo, historia imerekodi kwamba kanisa la kwanza lilifundisha dhidi ya matumizi ya ala hizo za muziki, kama ambavyo pia wale wabadilishi wakuu wa kanisa wa siku ambazo zilipita pia walifundisha.

Kwa habari zaidi kuhusu matumizi ya ala za muziki katika ibada za kanisa tazama toleo la 21 hapo kwenye www.thegospeltruth.org

Je, Bwana amekubali njia za kisasa za kufanya ibada za sifa kanisani?

Kuna mambo kadhaa ambayo yanahusika katika swali hili, na pengine sitaweza kuyashughulikia mambo yote yaliyomo; lakini hapa nitashiriki mambo kadhaa ya kuwaza kuhusu njia za kisasa zinazotumiwa kufanya “ibada za sifa.” Kwanza kabisa tunahitaji kutambua kwamba sifa na ibada ni mambo ambayo yameamriwa na Bwana. Lakini sifa na ibada zilizo za kweli ni mambo ambayo yanaongozwa na Roho na sio ya kimwili. Kuna makanisa mengi ambayo huwa na sherehe zinazofanana na michezo ya kuigiza na ambazo huwa ni za kuchangamsha mwili, na katika sherehe hizo kunafanyika humo kanisani mambo ambayo hayana faida kwa hali bora ya nafsi ya Mkristo. Kama watu watajifurahisha kimwili kwenye ukumbi wenye mataa yanayo-mulika-mulika, na wanatumia bedi za kimuziki, na kupiga rumba huku wakiimba nyimbo za kumsifu Mungu, halafu baadaye wakarudi katika maisha yao ya dhambi hapo nyumbani mwao, kukubalika kwa jambo kama hilo ni kitu ambacho sisi tunatilia shaka sana. Si jambo ambalo linawezekana tu, bali pia ni ukweli kwamba nyingi za sifa na ibada za kisasa huwa ni jambo la kufunika maisha ya dhambi tu na kisingizio kuwa mtu anaishi kama Mkristo.



Yule ambaye tunastahili kuabudu kwa kweli ni Kristo mwenyewe. Nyingi za sifa na ibada za kisasa hutukuza na kusherehekea vipaji vwa wanadamu na uwezo wao wa kimwili. Washiriki wa ibada hizo hupata kuchangamshwa kihisia kwenye ibada hizo, lakini mimi mwenyewe sijawahi kuona utakatifu kuwa ni matokeo bora ya baadaye ya ibada kama hizo. Kusema kweli muziki ukiwa peke yake sio ibada, na ikiwa sifa na ibada zetu ni “jambo la kihisia tu” (kama ambavyo mwandishi mmoja alisema), basi pengine hizo sio ibada za kweli.

Kumwabudu Mungu ambako kunakubalika ni kule kunakotokana na moyo ambao umejaa upendo kwake Mungu, nao moyo huo wa upendo hudhibitika kwa mtu kuwa mtiifu kwa Mungu. Hata katika nyakati za Yesu kulikuwa na wale ambao walimkaribia Yesu kwa vinywa vyao na kumheshimu kwa midomo yao tu, ilhali mioyo yao ilikuwa mbali naye (Mathayo 15:18).

Matendo mengi ya ibada za sifa za za kisasa huwa ni ya kidunia, na huwa kinyume na urahisi wa ibada za kiungu. Hata ingawa kila mtu ana haki na mweke wa kumsifu Mungu, watoto wa Mungu hawastahili kufanya kosa la kukuza au kuvumilia mazoea ambayo hayakubaliki mbele zake Bwana. Ni jambo la kusikitisha kwamba kwa kawaida ibada za kisasa (za sifa) hazivuti watu ili kutaka kuwa na uhusiano wa karibu na Bwana wao.



JE, WAJUA?

Katika 1 Timotheo 2:9, kabla Mtume Paulo kutoa amri kwamba wanawake wadumishe viwango vinavyokubalika wanapovaa mavazi, na pia kwamba wawe na tabia nzuri (mafundisho ambayo wengi wa washiriki wa kanisa la utakatifu hukubaliana nayo), mtume huyu alishauri kuhusu wanaume: “Basi, nataka wanaume wasalishe kila mahali, huku wakiinua mikono iliyotakata pasipo hasira wala majadiliano.”



VAZI LA SIFA

[Bwana ametupatia] *mafuta ya furaha badala ya maombolezo, vazi la sifa badala ya roho nzito.* — Isaya 61:3

Yesu Kristo alikuja kuleta habari njema kwa ulimwengu uliokuwa mgonjwa kutokana dhambi. Yeye alileta uponyaji wa kiroho na ukombozi kwa nafsi ambazo zilikuwa zaelekea Yehanamu. Mahali ambamo kulikuwa na maombolezo na huzuni sasa kukapatikana furaha na amani. Mahali ambapo kulikuwa na uzito wa moyo na hali ya kugandamizwa sasa Bwana akatoa vazi la sifa.

Wanadamu huwa na uchaguzi wa kufanya, ikiwa watadumisha uzito wa mioyo huku wakiwa dhambini, au watafungua mioyo yao inayobeba mizigo mizito na kumruhusu Yesu kuwapa pumziko na amani. Shauku la Bwana ni la kuwavalisha watoto wake vazi la sifa ambalo huleta utukufu na heshima kwake Baba.

Ni jambo muhimu tukumbuke kwamba wakovu hautukomboi kutokana na uchungu wote wa moyo ambao huletwa na kuwepo kwa dhambi ulimwenguni. Kungali kuna uwezekano kwamba watu walio-okoka watapatwa na matatizo ya kimwili, ya kihisia, na shida zingine ambazo hazitadumu sana. Lakini katikati mwa shida hizo adui yetu angependa kuzamisha watoto wa Mungu kwenye dimbwi la moyo mzito wenye kulemewa na mizigo mizito, mahali ambapo watu hupoteza tumaini na kudumu katika giza nyingi. Yesu alikuja ili kuwafariji waombolezaji na pia kuwahudumia wale ambao wanaungua.



Wakati roho wa uzito anapotaka kukukalia, wewe Mkristo mtazame Bwana ili upate kuona mikono yake ambayo imenyoosha kwako kupitia kwa vazi la sifa. Hata wakati kuna giza kubwa, wakati ambapo kuna uchungu mwingi, unaweza kushinda moyo wako uliolemewa na mizigo mizito kwa njia ya roho wa kusifu. Wakati mambo yanayokuzunguka yanapoenda mrama, ungali unaweza kumsifu Bwana kwa ajili ya wokovu wake na hata upendo wake. Unapomsifu Mungu wingu la kukata tamaa linaweza kuvutwa kwa nyuma likapata kukuondokea. ■

Anwani

The Gospel Truth
P. O. Box 2042
Nixa, MO 65714
USA

Email:
editor@thegospeltruth.org

UTAKATIFU KWA BWANA